Tangazo la Serikali Na ……………………. La Tarehe……......…………

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO**

**(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))**

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA, 2018

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1 | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Eneo la Matumizi | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. |
| Tafsiri | 3 | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo;- |

**"Ada na ushuru"** maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Kwa ajili ya ada, huduma, vibali. au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"**Afisa Masuuli"** maana yake ni Mkurugenzi au Afisa yeyote atakayeidhinishwa kutekeleza majukumu kwa niaba ya Mkurugenzi.

**"Afisa Muidhiniwa"** maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo hizi.

**"Bidhaa"** maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa .

**"Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

**"Kibali"** maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

**"Leseni ya biashara"** maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, Kampuni au Taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri.

**“Machinjio”** maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

**“Matangazo ya biashara**“ maana yake ni ishara, alama, maneno, yaliyobandikwa kwenye mabango, kuta za nyumba au vibao kwa lengo la kuitangaza biashara fulani .

**“Masoko“** maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuzia na kununulia bidhaa.

**“Mkurugenzi “**maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa kutekeleza majukumu kwa niaba yake.

**“Sheria”** maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290.

**“Soko”** maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko kwa ajili ya huduma ya umma.

**“Stakabadhi”** maana yake ni stakabadhi ya kieletroniki itakayotolewa na Halmashauri kama uthibitisho wa malipo ya ada au ushuru.

Mamlaka ya Halmashauri kutoza Ada na Ushuru

4 (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika biashara, huduma, vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu cha 4(1) cha cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-

i. Machinjio, ukaguzi wa nyama
ii. Biashara ya mazao ya biashara na chakula
iii. Pango au matumizi ya majengo ya Halmashauri
iv. Masoka na magulio
v. Minada
vi. Usajili wa magari ya biashara na mizigo
vii. Mitambo, mwalo na makarasha
viii. Malori ya makaa ya mawe
ix. Minara ya simu na redio
x. Nyumba za kulala wageni
xi. Vibali vya ujenzi
xii. Huduma za ardhi
xiii. Vitalu vya miche na mashamba ya mbegu

xiv. Matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti, wapiga mziki, waonyesha video au sinema
xv. Mazao ya miti ya kupandwa
xvi. Kumiliki silaha
xvii. Stendi na maegesho ya magari, bajaji na pikipiki (bodaboda)
xviii. Leseni za vileo
xix. Usajili wa vikundi vya kijamii
xx. Biashara ya mazao ya nyuki

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ushuru wa Matangazo ya biashara kwa njia ya vipaza sauti | 5 | 1 | Kila mfanya biashara au mtoa huduma atakayetangaza biashara au huduma yake kwa kutumia vipaza sauti atatakiwa kulipa ushuru wa matangazo kwa viwango vilivyooneshwa katika jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi baada ya kupewa kibali. |
| | | 2 | Ni marufuku kwa mfanyabiashara au mtoa huduma yeyote kutumia matangazo ya vipaza sauti kwa nia ya kudhalilisha, kufedhehesha mtu, watu, kikundi cha watu, biashara au huduma ya mtu mwingine. |
| Usajili na ushuru wa vitalu vya miche na mashamba ya mbegu | 6 | 1 | Halmashauri itakuwa na jukumu la kusajiri na kusimamia vitalu vyote vitakavyo kuwa vinazalisha miche na mashamba ya kuzalisha mbegu ambavyo vitakuwa vinamilikiwa na vikundi, kampuni, vyama na watu binafsi. |
| | | 2 | Halmashauri itakuwa inatoza ada ya usajili na ushuru wa vitalu vya miche na mashamba ya mbegu kwa gharama kama ilivyo ainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi. |
| Usajili wa biashara, magari ya biashara na mizigo, bodaboda, mitambo na minara | 7 | 1 | Halmashauri itaweka utaratibu wa kusajili biashara, magari ya mizigo, magari ya abiria, pikipiki, mitambo mbalimbili na minara ya simu pamoja na ya redio katika eneo lake la utawala kwa utaratibu kama ulivyo ainishwa katika Sheria Ndogo hizi. |
| | | 2 | Halmashauri itatoza Ada au Ushuru katika biashara na vitu vyote vilivyosajilwa kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) cha Sheria ndogo hizi kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mamlaka na uwezo wa Halmashauri kufunga biashara | 8 | | Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuamuru kufunga biashara yoyote ya mmiliki au mtumiaji wa huduma yoyote baada ya kutoa notisi endapo mmiliki au mtumiaji atakataa kulipa ada, ushuru au kibali kama ilivyoorodheshwa chini ya Sheria Ndogo hizi. |
| Namna ya kukusanya Ada na Ushuru | 9 | 1 | Malipo ya Ada au Ushuru yatakayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kukatiwa stakabadhi halali ya kielekroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika. |
| | | 2 | Malipo yatathibitishwa kwa kuonyesha stakabadhi ya Halmashauri na kwamba utetezi ambao sio wa njia ya stakabadhi hautakubalika kwa ajili ya kuthibitisha malipo kwa Halmashauri. |
| | | 3 | Isipokuwa kwamba risiti ya aina nyigine inaweza kukubalika iwapo Halmashauri au wakala, kwa sababu zisizozuilika, itashindwa au atashindwa kutoa risiti ya kielektroniki kwa wakati huo na mazingira ya wakati na mahali hapo haitakuwa imetolewa kutokana na sababu ambazo Halmashauri itatolea ridhaa yake. |
| | | 4 | Ada au Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali. |
| Mamlaka ya Kukamata mali au bidhaa. | 10 | 1 | Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yoyote endapo atashindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | 2 | Endapo bidhaa au mali itakayokamtwa na Halmashauri au wakala haitolipiwa Ada au Ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa kwa mali zinazoharibika haraka, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza bidhaa au mali hizo kwa njia ya mnada na fedha zitakazopatikana zitawekwa kwenye akaunti ya Halmshauri. |
| | | 3 | Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kuhusiana na mali au bidhaa iliyokamatwa katika kutekeleza Sheria Ndogo hizi bila kwanza kupata idhini ya maandishi ya Afisa Masuuli. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 4 | Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada na ushuru kwa njia ya Mahakama. |
| | | 5 | Halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa hasara itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zilizokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri isipokuwa kama hasara au uharibifu huo umetokana na uzembe au utendaji kazi usioridhisha wa mtumishi wa Halmashauri au wakala. |
| Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru | 11 | 1 | Kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru anawajibu wa kulipa Ada au Ushuru huo kwa utaratibu na viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi. |
| | | 2 | Ni wajibu wa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru. |
| | | 3 | Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu anayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo yote aliyofanya. |
| Kibali au leseni | 12 | 1 | Ni wajibu wa kila mfanyabiashara au mtu yoyote anayetaka kufanya biashara au jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri |
| | | 2 | Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | 3 | Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya biashara katika eneo lolote lililopo chini ya mamlaka ya Halmashauri bila kuwa na leseni au kibali. |
| Mamlaka ya Halmashauri kuteua wakala | 13 | | Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteuwa mtu, Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ada au Ushuru kwa niaba yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi |
| Wajibu wa wakala | 14 | 1 | Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa na wajibu waKukusanya na kupokea Ada au Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango |

kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

2 Wakala atakusanya Ada au Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

**Makosa na adhabu kwa wakala** 15 Itakuwa ni kosa kwa wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) atakusanya Ada au Ushuru bila idhini ya Halmashauri.

(2) atakusanya Ada au Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada au Ushuru kilichokubaliwa katika mkataba wa kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atashindwa kutoa stakabadhi halali ya malipo kwa Ada au Ushuru aliokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wakala akipatikana na hatia atapata adhabu kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 18 (1) cha Sheria Ndogo hizi.

**Uwezo wa Afisa mwidhiniwa** 16 Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya, kufanya tathimini au jambo lolote linalohusiana na Ada, Ushuru, Leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

**Makosa** 17 Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-

(1) Atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashuri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataaa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(3) Atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza

majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.

(5) Atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(6) Atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Adhabu

18 (1) Mtu yoyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tshs.200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tshs.1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili lakini kizichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kutokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi atawajibika kuilipa Halmashauri gharama za ukamataji na hasara na usumbufu mwingine wowote utaojitokeza.

Uwezo wa Mkurugenzi Kufifilisha kosa

19 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyooneshwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa Ada au Ushuru anaopaswa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

**JEDWALI LA KWANZA**
**Chini ya Kifungu cha 4(1)**

**SEHEMU YA KWANZA**

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (i, ii)**

**I. ADA YA UKAGUZI WA NYAMA**

| S/NO | Mnyama | Idadi | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 1 | 1,000/= |
| 2 | Mbuzi / Kondoo | 1 | 800/= |
| 3 | Nguruwe | 1 | 1,000/= |

**II. KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO**

| S/NO | AINA YA ZAO | KIASI (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 200,000/= kwa kila msimu |
| 2 | Maharagwe | 200,000/= kwa kila msimu |
| 3 | Mazao mengine ya biashara na chakula | 50,000/= kwa kila zao kwa msimu |

**III. USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO**

| S/NO | AINA YA ZAO | USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 2% ya bei ya kununua |
| 2. | Mchele/mpunga | 2% ya bei ya kununua |
| 3. | Maharage | 2% ya bei ya kununua |
| 4. | Karanga | 2% ya bei ya kununua |
| 5. | Alizeti | 2% ya bei ya kununulia |
| 6. | Miwa | 2% ya bei ya kununulia |
| 7 | Mazao mengine ambayo Hayakutajwa | 2% ya bei ya kununulia |
| 8 | Kahawa,Korosho,Tumbaku | 3% Mazao ya biashara ya bei ya kununua |

**SEHEMU YA PILI**

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (iii)**

**I. KODI YA PANGO VIBANBA VYA HALMASHAURI**

| S/.No | Aina ya jengo | Kodi ya pango (Tshs) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Vibanda vya gereji | Tshs. 30,000/= | Kwa mwezi |

### II. ADA YA HUDUMA YA CHOO /BAFU

| S/NO | AINA YA JENGO | ADA (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Choo cha soko kuu | 200/= kwa mtu mmoja |
| 2. | Choo/Bafu cha biashara kinachomilikiwa na Halmashauri | 200/= kwa mtu mmoja |

## SEHEMU YA TATU

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (iv)**
**USHURU WA MASOKO/ GULIO**

| S/No | Aina ya bidhaa | Ushuru (Tshs) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Nguo za mitumba | 500/= | Kwa siku |
| 2. | Nafaka rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 3. | Madawa asili | 500/= | Kwa siku |
| 4. | Migahawa ndani ya soko | 500/= | Kwa siku |
| 5. | Samaki rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 6. | Mboga za majani | 500/= | Kwa siku |
| 7. | Dagaa rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 8. | Wauza vyungu | 500/= | Kwa siku |
| 9. | Miwa rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 10. | Matunda/ nyanya/ vitunguu | 500/= | Kwa siku |
| 11. | Viatu rejareja | 500/= | Kwa siku |
| 12. | Bidhaa nyinginezo | 500/= | Kwa siku |
| 13. | Bidhaa nyingie pamoja na mazao ya kilimo. | 500/= | Kwa siku ya gulio tu |

## SEHEMU YA NNE

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (v)**
**USHURU WA MINADA**

| S/NO | AINA YA MNYAMA | USHURU (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | Ng’ombe | 5,000/= | Kwa kila Ng’ombe |
| 2 | Mbuzi /Kondoo | 1,500/= | Kwa kila mbuzi /kondoo |

**SEHEMU YA TANO**

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (vi)**
**ADA YA USAJILI WA MAGARI YA BIASHARA NA MIZIGO**

| S/No. | Aina ya gari | Ada (Tshs) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Taxi | 40,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | Pick Ups | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Trekta | 60,000/= | Kwa mwaka |
| | Lori au Basi 3.5 tani-7 | 50,000/= | Kwa Mwaka |
| 4. | Lori za biashara tani 8-10 | 70,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | Lori za Biashara tani 11 na kuendea | 100,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Bajaji | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 7. | Bodaboda | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 8. | Noah | 40,000/= | Kwa Mwaka |

**SEHEMU YA SITA**

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (vii)**
**USHURU WA MITAMBO, MWALO NA MAKARASHA**

| **S/NO** | | **USHURU (Tsh)** | **MUDA** |
|---|---|---|---|
| 1 | PLANT (KUCHENJUA MCHANGA WA DHAHABU | 7,000,000 | KWA MWAKA |
| 2 | MWALO | 40,000-Usajili<br>200,000-Ada | Mara moja<br>KWA MWAKA |
| 3 | KARASHA | 20,000-Usajili | Mara moja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 100,000-Ada | KWA MWAKA |
| 4 | MAWE YA DUARA | 1,000 | MFUKO kwa Mwaka |

## SEHEMU YA SABA

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (viii)**
**USHURU WA MALORI YA MAKAA YA MAWE**

| S/NO | AINA | USHURU (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1. | LORI | 1,000/= | Kwa Tani moja |
| | | | |

## SEHEMU NANE

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (ix)**
**MINARA YA SIMU NA REDIO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Minara<br>• Kibali cha ujenzi wa mnara wa simu<br>• Kibali cha ujenzi wa mnara wa Redio<br>• Ushuru wa mnara wa simu<br>• Ushuru wa Mnara wa Radio | Tshs. 1,500,000/= Mara moja tu<br>Tshs. 1,500,000/= Mara moja tu<br>Tshs. 5,000,000/= kwa mwaka<br>Tshs. 500,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU TISA

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (x)**
**USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI**

| S/NO | AINA YA GESTI | USHURU | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | GESTI ZOTE | Asilimia 10% kwa kila kitanda | Kwa siku |

## SEHEMU KUMI

### Chini ya kifungu cha 4 (2) (xi)
### KIBALI CHA UJENZI

| S/NO | Aina ya jengo | Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ghorofa 1 | 120,000/= |
| 2. | Ghorofa 2 na kuendelea | 150,000/= |
| 3. | Nyumba za biashara | 50,000/= |
| 4. | Ghala au bohari | 200,000/= |
| 5. | Kituo cha mafuta | 500,000/= |
| 6. | Nyumba za makazi | 10,000/= |
| 7. | Nyumba za makazi na biashara | 30,000/= |
| 8. | Majengo mengine ambayo hayakutajwa hapo juu | Itategemea aina ya jengo |

## SEHEMU KUMI NA MOJA

### Chini ya kifungu cha 4 (2) (xii)
### I. ADA YA KUBADILISHA MATUMIZI YA ARDHI, KUGAWA VIWANJA, MASHAMBA AU KUBORESHA MCHORO

| S/N | MATUMIZI YA AWALI | MATUMIZI YANAYOOMBWA | KIASI (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | Makazi na biashara | 50,000/= |
| 2 | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja | 50,000/= |
| 3 | Makazi pekee | Shule ,Hosteli,Zahanati na huduma nyinginezo za jamii | 50,000/= |
| 4 | Makazi pekee | Hoteli | 150,000/= |
| 5 | Makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 500,000/= |
| 6 | Makazi na biashara | (Maduka makubwa )<br>Super Market/Shooping Mall | 200,000/= |
| 7 | Makazi pekee | (Viwanda/huduma)<br>Service Trade/Industrial | 200,000/= |
| 8 | Makazi pekee | Ghala (Yard/Godown) | 100,000/= |
| 9 | Biashara | Makazi | 20,000/= |
| 10 | Kugawa shamba kuwa viwanja vya makazi | makazi | 50,000/= |
| 11 | Kugawa kiwanja cha makazi | makazi | 50,000/= |
| 12 | Kugawa kiwanja kwa | biashara | 200,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | matumizi ya hoteli | | |
| 13 | Jengo lolote ambalo halijatajwa | | Itategemea aina ya jengo |

### II. ADA YA KUCHANGIA UPIMAJI WA VIWANJA/MASHAMBA

| S/NO | Aina ya uwanja | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Kuuza Kiwanja cha Halmashauri – kimoja | 100,000/= |
| 2 | Upimaji wa mashamba(kwa Heka) | 100,000/= |

## SEHEMU KUMI NA MBILI

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xiii) Na 7(2)**

**ADA YA USAJILI NA USHURU WA VITALU VYA MICHE NA MASHAMBA YA MBEGU**

| S/NO | AINA | ADA YA USAJILI | USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Vitalu vya miche | Tshs.10,000/= kwa mwaka | 3% ya bei ya kuuzia mche |
| 2. | Shamba la Mbegu | Tshs.50,000 kwa mwaka | 2% ya bei ya kuuzia mbegu kwa kilo. |

## SEHEMU KUMI NA TATU

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xiv)**

**USAJILI, KIBALI NA USHURU WA MATANGAZO YA BIASHARA KWA NJIA YA VIPAZA SAUTI, WAPIGA MZIKI, WAONYESHA VIDEO AU SINEMA**

| S/NO | | KIASI (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha matangazo ya biashara | 20,000/= | Kila tangazo |
| 2 | Usajili wa waonyesha video/sinema | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usajili wa wapiga Muziki ndani ya Halmashauri | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Kibali cha kupiga mziki kwa wenye vyombo vya muziki ndani ya Halmashauri | 10,000/= | Kwa kila tukio |
| 5 | Kibali cha kupiga mziki kwa wenye vyombo vya muziki kutoka nje ya Halmashauri. | 20,000/= | Kwa kila tukio |

**SEHEMU KUMI NA NNE**

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xv)**

**USAJILI WA BIASHARA NA USHURU WA MAZAO YA MITI YA KUPANDWA**

| S/NO | Aina ya zao | Kiasi (Tshs) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkaa | 1,000/= | Kwa gunia moja |
| 2 | Vifaa vilivyotengenezwa kwa mbao<br>• Shata za milango<br>• Fremu za milango/madirisha<br>• Viti/stool<br>• Kitanda<br>• Seti ya kochi<br>• Vikapu/mikeka<br>• Ubao uliochanwa<br>• Mabanzi<br>• Kuni $m^3$ 1<br>• Uuzaji miche ya miti-viriba<br>-wazi | 6,000/=<br>5,000/=<br>1,000/=<br>6,000/=<br>15,000/=<br>300/=<br>5,000/=<br>300/=<br>200/=<br>100/= | Kwa kimoja |
| 3 | Maombi ya Transit Pass.<br>• Gari chini ya Tani 7 (saba)<br>• Gari zaidi ya Tani (saba) | 5,000/=<br>10,000/= | |
| 4 | Usajili wa biashara ya mazao ya miti ya kupandwa.<br>• Mbao<br>• Magogo<br>• Nguzo<br>• Fito<br>• Duka bidhaa za misitu<br>• Mkaa<br>• Kuni<br>• Furniture mart | 50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/=<br>50,000/= | Kwa mwaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | • Saw mill<br>• Fundi seremala<br>• Madawa asili/kuranda/kuchana mabo<br>• Mashine ya kuchakata mbao | 50,000/=<br>10,000/=<br>10,000/=<br>50,000/= | |

## SEHEMU KUMI NA TANO

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xvi)**
**ADA YA KUMILIKI SILAHA**

| S/NO | Aina ya ada | Kiwango (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Kumiliki Silaha (Gobore) | 4,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU KUMI NA SITA

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xvii)**
**USHURU WA STENDI YA BASI**

| S/NO | AINA YA GARI | USHURU (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabasi /malori | 2,000/= | Kwa siku |
| 2. | Hiace | 1,000/= | Kwa siku |
| 3. | Taxi | 500/= | Kwa siku |
| 4. | Bajaji | 500/= | Kwa siku |
| 5. | Bodaboda | 200/= | Kwa siku |
| 6. | Noah | 1,000/= | Kwa siku |

## SEHEMU KUMI NA SABA

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xviii)**
**LESENI YA VILEO**

| S/NO | | USHURU (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1. | Wauzaji wa jumla | 20,000/= | Kwa miezi 6 |
| 2. | Baa | 40,000/= | Kwa miezi 6 |
| 3. | Grocery | 30,000/= | Kwa miezi 6 |
| 4. | Pombe za kianyeji | 12,000/= | Kwa miezi 6 |
| 5. | Ada ya Maombi | 2,000/= | Kwa Kila anayetaka Leseni ya Vileo |

## SEHEMU KUMI NA NANE

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xix)**
**USAJILI WA VIKUNDI**

| S/NO | | KIASI (Tshs) | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Usajili wa kikundi cha Kijamii | 20,000/= | |
| 2 | Ada ya kikundi Kikubwa | 15,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Ada ya kikundi kidogo | 5,000/= | Kwa mwaaka |

## SEHEMU TISA

**Chini ya kifungu cha 4 (2) (xx)**
**MAZAO YA NYUKI**

| AINA YA MALIPO | KIASI (Tshs) | IDADI |
|---|---|---|
| Ada na usajili | 50,000/= | Kwa mwaka |
| Ushuru wa asali | 300/= | Kwa kilo moja |

## JEDWALI LA PILI

## HATI YA KUFIFILISHA KOSA
**(Chini ya kifungu cha 19)**

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya………………………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwamba mnamo tarehe……ya mwezi……………..mwaka …………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga za mwaka 2018

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………………ya mwezi…………………Mwaka………………………..
Jina…………………………………..
Saini………………………………….

Mbele ya:
Jina………………………………………..
Cheo………………………………………
Saini………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 13 ya mwezi Julai mwaka 2018 mbele ya:-

JUMA A. MNWELE
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga

AMBROSE MTARAZAKI NCHIMBI
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga

NAKUBALI

Dodoma, **M**HE. SELEMANI. S. JAFO (MB)
……………………2018 WN-OR-TAMISEMI